

## **LEARNING BY EAR**

### **“The Lost Kid – the Story of Single Mothers in Africa”**

#### **EPISODE 3: “More than just a Game”**

**AUTHOR: Mantegaftot Sileshi Siyoum**

**EDITOR: Stefanie Duckstein, Adrian Kriesch**

**PROOFREADER: Kate Hairsine**

#### **List of characters by scene:**

##### **SCENE ONE: DAY TIME AT THE LOCAL MARKET**

- Askale (f,21)
- Kassech (f, 22)
- Buyer: (f, 58)
- Narrator (m, around 35)

##### **SCENE TWO: AFTERNOON IN JONAS' VILLAGE**

- Jonas (m,15)
- Mekete (m,16)
- Challa (m,17)
- Aster (f, 15)
- Narrator (m, around 35)

##### **SCENE THREE: AT NIGHT AT KASSECH'S HOUSE**

- Kassech (f, 22)
- Begidu (m, 7)
- Narrator (m, around 35)

#### **SCENE FOUR: AT NIGHT AT ASKALE’S HOUSE**

- **Askale (f,21)**
- **Samy (m, 6)**
- **Narrator (m, around 35)**

## **INTRO:**

Hamjambo, wapendwa wasikilizaji! Karibuni kwenye sehemu ya tatu ya kipindi chetu cha mchezo wa redio cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako kiitwacho “MWANA MPOTEVU- KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”. Katika sehemu iliyopita, Jonas na marafiki zake wawili wameamua kumuibia Bwana Kasu ambaye ni tajiri mkubwa katika kitongoji wanachoishi. Aidha, marafiki wawili kina mama wachanga, Askale na Kassech wamegombana baada ya Askale kumwambia Kassech kumtunza vyema mwanawe Begidu. Ebu tuone yatakayotokea katika sehemu ya leo iitwayo “SI MCHEZO”. Tunakutana na kina mama hao wawili sokoni wanakouzia bidhaa zao.

## **SCENE ONE: DAY TIME AT THE LOCAL MARKET**

- 1. ATMO: LOCAL MARKET, ATMO OUTSIDE, TRAFFIC NOISES**

*KW begin*

- 2. Buyer:** Mkaa huu unaonekana mzuri.
- 3. Kassech:** Naam! Ni mti wa mkaratusi. Shika hapa. Shikilia huo mfuko wako tafadhali.
- 4. SFX: CHARCOAL THROWN INTO A PLASTIC BAG**
- 5. Buyer:** Pesa zako hizi.
- 6. SFX: COINS DROPPING INTO HANDS**

7. **Buyer:** Hakuna nyongeza jamani! Mimi ni mteja wako wa muda mrefu.
8. **Kassech:** Najua, lakini mwenyewe unafahamu, vitu vingi vimepanda bei siku hizi. Hata hivyo, shika kiasi hiki kidogo.
9. **SFX:** **CHARCOAL THROWN INTO PLASTIC BAG**
10. **Buyer:** **(as she leaves)** Asante! Nitakuja tena kesho.

*KW end*

11. **Askale:** **(comes close)** Sijapata mtu wa kununua mkate wangu. Leo ni siku yako, Kassech. Unakaribia kumaliza mkaa wako yote.
12. **Kassech:** **(Adamant)** Naam, Askale.
13. **Askale:** Samahani kwa ugomvi wa jana.
14. **Kassech:** Ni sawa!
15. **Askale:** Wajua, mwanangu Samy anaendelea kufanya vizuri shuleni.
16. **Kassech:** **(without interests)** Naam.

**17. Askale:** Nilikutana na mwalimu wa masomo yetu ya

**Formatiert:** Nummerierung und Aufzählungszeichen

jioni akaniuliza kukuhusu. Kwa nini hujarudi masomoni?

**18. Kassech:** **(Angrily)** Kwa hisani yako, shughulika na mambo yako! Ninapouza mkaa, hela nipatazo zinatasha kodi na kumnunulia mwanangu vitu anavyovihitaji! Hivyo vyatosha!

**19. Askale:** Sawa! Sawa!

**20. NARRATOR:** Askale ana wasiwasi kwa sababu urafiki wake wa dhati na Kassech unaendelea kuingia dosari kwa kuwa kila mara anampa Kassech ushauri wa jinsi ya kumlea mwanawe. Kassech haoni sababu inayomfanya Askale kumwambia mara kwa mara namna ya kumlea mwanawe, Begidu. Kwengineko, Jonas, mdogo wake Kassech anakaa barazani akicheza karata na marafiki zake wawili, Challa na Makete.

## **SCENE TWO: AFTERNOON IN THE SUBURB**

**21. SFX:** **OUTSIDE, THUNDER AND BOLT IN THE DISTANCE**

**22. SFX:** **SHUFFLING, CARDS BEING MIXED**

**23. Jonas:** Hali hii ya hewa haileweki!

**24. Challa:** Naam, ni vigumu kutabiri wakati mvua

itakapoanza kunyesha.

25. **Mekete:** Si hoja! Mvua ikianza kunyesha tutatafuta pa kujikinga. Jamani tusishughulishwe na mvua. Tuendeleo na mchezo. Kadi zenu hizi.
26. **SFX:** **FLIP OVER CARDS**
27. **Challa:** Jamaa, Tazameni kule!
28. **Mekete:** Nini! Alaa! Aster.
29. **Challa:** Mjukuu wa Papa Tilahun!
30. **Mekete:** **(panics)** Na je akijua kuwa tulipanga kumwibia babu yake?
31. **Challa:** Taratibu! Usiseme kwa sauti! Anakuja huku tulipo!
32. **SFX:** **FOOTSTEPS APPROACH**
33. **Aster:** Jonas, mambo!
34. **Jonas:** **(Nervous)** Poa! A...A...Aster.
35. **Mekete and Challa: (Giggling).**
36. **Aster:** Ushasikia yaliyompata mpwa wako?
37. **Jonas:** Hapana, kwani Begidu alifanyika nini?

- 38. Aster:** Siku mbili zilizopita, nilimpata jikoni kwetu.  
Mvua ilikuwa ikinyesha na kulikuwa na baridi  
kali. Alikuwa amelala karibu sana na moto!
- 39. All Three:** Nini?
- 40. Aster:** Kweli, ninayokwambia. Dadako hakuwa  
nyumbani.
- 41. Jonas:** Huyo ni mpumbavu!
- 42. Aster:** Kisha, nilimbeba nikamlaza kitandani nyumbani  
kwetu.
- 43. Jonas:** Asante! Kwa hisani yako mtunze vizuri.
- 44. Aster:** Sawa. Kwaheri!
- 45. Jonas:** Kwaheri!
- 46. SFX: FOOTSTEPS LEAVE**

***KW begin***

- 47. Challa:** (**teases Jonas**) Uiiii. Laiti angekulaza wewe  
kitandani, Jonas.
- 48. Mekete:** (**Laughs**) A...A...Aster!
- 49. Both:** (**Laugh**)
- 50. Jonas:** Ebu niachenii!



***KW end***

**51. SFX: STARTS TO RAIN**

**52. SFX: FOOTSTEPS OF THE THREE BOYS LEAVE**

**53. NARRATOR:** Wakati Aster anapoondoka kuelekea upande mmoja, vijana hao watatu wanaelekea upande wa pili kujikinga mvua inayoanza kunyesha ghafla. Usiku huo, Kassech kwa mara nyingine tena anatatizwa na shida za Begidu. Mwanawe ameanza mwaka wake wa kwanza shuleni na hafanyi vyema. Kama kawaida huko nyumbani, Kassech hawezi kuzungumza vyema na mtoto wake kuhusu matatizo anayoyapata shuleni.

### **SCENE THREE: AT NIGHT AT KASSECH'S HOUSE**

**54. SFX. FLIPPING PAPERS**

**55. Kassech:** **(Angrily)** Mbona umefanya vibaya hivi?  
Angalia, huu mchoro wa nini?

**56. Begidu:** **(With fear)** Huyu ni paka.

**57. Kassech:** **(Mocking at him)** Sema kwa Kiingereza "It is a cat." Ebu zitaje herufi za neno CAT!

**58. Begidu:** K...A...T

**59. Kassech:** **(Very angry)** Nini K...A...T...?

**60. Begidu:** Cat.

- 61. Kassech:** Hapana! Sivyoy! (**spells the letters**) K...A...T...!  
Inapaswa kuwa, C...A...T! Ebu nikwambie,  
tumia muda wako mwingi ukijifunza haya  
mambo badala ya kurandaranda kila mahali  
ukiwambia watu kuwa hupati chakula cha  
kutosha! Mshenzi wewe! Nenda kalale sasa!
- 62. Begidu:** Mama, kwa nini unapenda kunitukana na  
kunipiga kila mara?
- 63. Kassech:** Usinijibu mimi! Nasema, uende ukalale.
- 64. Begidu:** (**He cries while he leaves**).
- 65. NARRATOR:** Kassech ana nini? Kwa hakika, si kwamba  
Kassech anamchukia mwanawe. Lakini kama kina mama wachanga  
wasiokuwa na waume, Kassech hajui jinsi ya kutunza mwanawe.  
Kassech anaonekana kulemewa na changamoto nyingi zinazomkabili  
kila siku. Kwa sababu ya kutatizika kote huko haelewi umuhimu wa  
malezi na elimu bora kwa makuzi ya mwanawe. Kadiri Kassech  
anavyoendelea kumtukana na kumpiga Begidu, ndivyo  
atakavyoendelea kuathiri ukuaji wake. Tofauti na Kassech, rafiki yake  
Askale analizingatia kwa dhati jukumu lake la ulezi wa mwanawe.  
Ndiyo sababu Begidu yumo kitandani akilia huku Samy na mamaye  
wakicheza na kucheka katika nyumba jirani.

### **SCENE THREE: AT NIGHT AT ASKALE'S HOUSE**

66. **SFX:** **NIGHT AMBIENCES**
67. **Askale:** **(Tickles Samy)**
68. **Samy:** **(Laughs)** Mama, Acha! Niache.
69. **Askale:** Wewe mwanangu mzuri! Sasa ni wakati wa...
70. **Samy:** Kusoma!
71. **Askale:** Naam, vizuri sana! Hata kama unasoma shuleni, unapaswa pia kujifunza kila siku jioni. Na unapojisomea, hebu nami nikapepete ngano ya kusaga unga wa kuoka mikate yangu. Sawa.
72. **SFX:** **POURING GRAINS ON A WINNOWING TRAY**
73. **Samy:** Sawa, Ma. Kesho ukioka mkate nami utanipa kipande?
74. **Askale:** Naam! Nina mikate hapa niliyorudi nayo kutoka sokoni. Sikuuza mikate yote leo. Kwani una njaa? Wataka mkate?
75. **Samy:** Hapana, si sasa, baadaye. Sasa nataka kusoma.
76. **Askale:** Asante mwanangu! Ebu niambie, kwa nini

kusoma ni muhimu?

- 77. Samy:** Sijui!
- 78. Askale:** Ili upate alama nzuri, mwanagu Samy. Lakini ukumbuke kwamba husomi kupata alama nzuri tu lakini pia unasoma ili ujisaidie maishani.
- 79. SFX:** **WINNOWERING THE GRAINS**
- 80. Askale:** Unaona, alama zako nzuri zinatokana na ushirikiano mzuri.
- 81. Samy:** Ushirikiano wetu?
- 82. Askale:** Naam Samy. Lau hukuniuliza mambo ambayo hukuelewa vizuri, na kama sikukueleza vizuri usingekuwa ukiyaelewa hayo mambo sasa. Unapaswa kuuliza vitu usivyovifahamu.
- 83. Samy:** Haya, naomba nikuulize kitu ambacho sielewi.
- 84. Askale:** Niulize!
- 85. Samy:** Kwa nini ninahudhuria shule? Mbona nisicheze na marafiki zangu huko nje?
- 86. Askale:** Wajua, unapokwenda shuleni, unajifunza mambo zaidi.
- 87. Samy:** Kwa nini marafiki zangu hawendi shuleni?

- 88. Askale:** Wanakwenda. Rafiki yako Begidu, kwa mfano, daima huhudhuria shule.
- 89. Samy:** Naam, lakini wengine hawendi shuleni. Kwa nini?
- 90. Askale:** Jamaa zao hawataki kuwapeleka.
- 91. Samy:** Mbona wasiwapeleke?
- 92. Askale:** Pengine hawana uwezo.
- 93. Samy:** Kwa nini hawana uwezo?
- 94. Askale:** Ewe Samy, unauliza maswali mengi.
- 95. Samy:** Lakini mama, umeniambia kuwa daima niulize kuhusu jambo lolote nisilolielewa.
- 96. Askale:** Naam, naam, unajua, wengi hawana fedha za kutosha kupeleka watoto wao shuleni.
- 97. Samy:** Na wewe una fedha za kutosha, ma?
- 98. Askale:** Nashukuru Mungu! Nilizo nazo zinatutosha sisi wawili.
- 99. Samy:** Na unapata vipi fedha za kututosha sisi wawili?
- 100. Askale:** Kutokana na mikate ninayooka kila siku nyumbani kisha kuiuza huko sokoni.
- 101. Askale:** **(Winnows).**

**102. SFX: WINNOWING THE GRAINS**

**103. Samy:** Ninaweza kukusaidia kupepeta ngano? Ili upate fedha zaidi!

**104. Askale:** **(laughs)** Asante sana Samy, zingatia masomo yako, na ukipata jambo usilolifahamu unieleze mara moja, sawa?

**105. Samy:** Sawa, ma, Nitakueleza.

**106. Askale:** Mtoto mzuri! **(Winnowing)**.

**107. SFX: WINNOWING THE GRAINS**

**OUTRO:**

Kama ujuavyo, marafiki wawili Askale na Kassech wana mambo mengi yanayofanana. Wao ni marika; hawakumaliza masomo yao ya shule na wote wanafanya kazi sawa ya kuuza bidhaa sokoni. Hata hivyo, malezi wanayowapa watoto wao hayafanani. Je hali hiyo itaishia wapi? Begidu atavumilia utepetevu wa mamake? Jiunge nasi kwenye sehemu itakayofuata ya mchezo wetu wa redio, **“Mwana Mpotevu- Kisa cha kina mama wawaleao watoto wao bila baba zao barani Afrika”**. Iwapo unataka kusikiliza kipindi hiki tena, au kuwasilisha maoni na mapendekezo yako, fungua ukurasa wa tovuti [dw.de/lbe](http://dw.de/lbe). Kwaheri!